Jarida La MELI

TOLEO LA 2. OKTOBA - DISEMBA 2021



DOWUTA yawafunda watumishi wa MSCL. UK. 2



MT SANGARA kurudi ziwa Tanganyika UK. 4



MV UMOJA yakabidhiwa Kwa Mkandarasi UK. 7



TPA YATAKIWA KUFANYA UHAKIKI WA NJIA KATIKA MAZIWA MAKUU NCHINI

Meli ya MV Mwanza ikiwa juu ya Chelezo ikiendelea na Ujenzi katika bandari ya Mwanza Kusini.

Na Edmond Rutajama

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa ameagiza Mamlaka ya Bandari nchini (TPA) kuona namna ya kutenga fedha kwa nia ya kufanya utafiti katika bandari za maziwa makuu ili ziweze kukidhi mahitaji ya meli zinazoendelea kujengwa nchini

Ametoa kauli hiyo wakati akizungumza na watumishi walio chini ya sekta ya ujenzi na uchukuzi baada ya mmoja wa wafanyakazi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) Mhandisi Abel Gwanafyo kumwelezea Waziri kuwa pamoja na ujenzi unaoendelea wa meli ya MV Mwanza lakini mazingira ya bandari za maziwa makuu hayana usalama wa kutosha kumsaidia nahodha wa meli kutia nanga bila woga.

Wakati akifafanua suala hilo Mhe. Prof. Mbarawa alisema kuwa kutokana na Serikali kuwekeza fedha nyingi katika kufufua na kujenga meli ni lazima njia na bandari za maziwa makuu zifanyiwe utafiti ili kuzalisha chati itakayoweza kuwaongoza manahodha katika kila bandari pamoja na kuweka minara ya ishara (signal towers) pamoja na maboya.

"Suala hili halihitaji muda mrefu, bandari hizi ziko chini ya TPA, TPA wana rasilimali za kutosha hili jambo watalifanya, hii itabidi tuwape kazi TPA wafanye wala sio serikali, TPA ina pesa za kutosha ya kufanya utafiti, kuweka minara ya ishara na maboya kwenye bandari zetu, haiwezekani tumejenga meli ya takribani Shilingi bilioni 90 kesho tunaipeleka pahala inakwenda kukaa tu haiwezekani'', Prof. Mbarawa alisisitiza.

Akiwasilisha hoja hiyo wakati wa kupokea maoni kutoka kwa watumishi hao, Mhandisi Gwanafyo alisema "Niwaeleze vizuri kwamba chombo chetu ni cha kisasa, meli ya ukubwa huo, lakini maziwa yetu yote Tanganyika, Victoria na Nyasa hayajafanyiwa utafiti, sasa hivi vyombo ni vipya na vikubwa usalama wa nahodha anapotaka kuongoza meli ni wasiwasi kwake anatumia uzoefu, kwahiyo ni tatizo Mheshimiwa Waziri tunaomba lifike kwako, suala la utafiti lichukuliwe uzito wa hali ya juu ili vyombo vyetu vitakapoanza kufanya kazi viende kwenye njia ambazo ziko salama".

DOWUTA YAWAFUNDA WATUMISHI WA MSCL



Katibu Mkuu DOWUTA taifa Ndg. Jonathan Msoma

Na Edmond Rutajama

Chama Cha Wafanyakazi wa Shughuli za Meli na Bandari (DOWUTA) kimewataka watumishi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) kufanya kazi kwa kujitoa kwa lengo la kuivusha Kampuni kutoka ilipo na kuwa yenye mafanikio zaidi katika kuwahudumia wananchi.

Hayo yamesemwa na Katibu Mkuu wa DOWUTA Ndg.Musoma katika kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa MSCL ambacho hufanyika kila robo mwaka ili kujadili maendeleo ya watumishi wa Kampuni hiyo pamoja na kutafuta njia za kutatua changamoto mbalimbali kwa mustakabali wa maendeleo ya Kampuni.

"Sisi kama wawakilishi wa wafanyakazi wajibu wetu ni kuwakumbusha wafanyakazi nini wajibu wao katika taasisi na kikubwa ni kuhakikisha taasisi haifi tena au hawarudi kule walikokuwa na katika kikao hiki tumetumia fursa ya kutuma salamu kwa wafanyakazi, wasifikirie sasa hivi ambapo tunajiendesha kwa meli mbili wakaanza kufikiria kuanza kupata maslahi zaidi watosheke kuona kwamba katika miaka miwili hawakuweza kupata mshahara, sasa maslahi madogo madogo yatakuja pale watakapoimarisha Kampuni" Musoma alisema.

Aidha, Katibu Mkuu huyo ameiomba serikali kuendelea kuiangalia na kuisaidia Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) mpaka pale itakapoweza kusimama yenyewe ili kuzuia kampuni hiyo isirudi katika hali yake ya awali.

"Nimefarijika na mwenendo wa kampuni ukizingatia taasisi tulipoitoa, tunasema tulipoitoa kwa sababu hii taasisi ilifikia mahala kwamba imekufa, Kampuni ilikuwa ikijiendesha kwa hasara , rai yetu bado tunasisitiza kwamba serikali waitazame hii Kampuni ili isirudi kule kwenye kufilisika kwa sababu Kampuni hii ni tegemeo kubwa kwa wananchi", Musoma alishauri.

Wakati huo huo Kaimu Mtendaji Mkuu wa MSCL Philemon Bagamilana aliwapongeza wafanyakazi wa Kampuni kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya ya kuhakikisha wanaifikisha Kampuni hiyo mbali na kuwataka wafanyakazi kuendelea kufanya kazi kwa bidii kwani kazi bado ni kubwa.

"Pamoja na changamoto tulizonazo, pamoja na madhaifu tuliyonayo, wafanyakazi wa kampuni ya huduma za meli tunafanya kazi kubwa sana, watendaji wa Kampuni ya Huduma za Meli wapo 135 tu, lakini hawa 135 ndio wanatoa taswira ya kuendesha hizi meli chache zilizopo haohao ndo wahangaike na miradi haohao 135 ndo wafanye shughuli zingine ambazo mnasikia tuanashiriki hatulali hakika wanafanya kazi kubwa sana", Bagambilana alisema.



Baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi MSCL wakisikiliza kwa makini mawasilisho mbalimbali wakati wa kikao hicho kilichofanyika katika ukumbi mdogo wa semina uliopo bandari ya Mwanza Kusini.

TASAC YAISHAURI MSCL BAADA YA UKAGUZI WA MRADI WA UJENZI WA MELI YA MV MWANZA



Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya TASAC wakiongozwa na Nahodha Musa Mandia wakimsikiliza kwa makini Mshauri Mwelekezi wa mradi wa ujenzi wa meli ya MV Mwanza kutoka kampuni ya OSK – ShipTech A/S Ndg. Rasmus Bayer (kushoto) wakati bodi hiyo ilipotembelea mradi huo.

Na Fatina Msangi

Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) ikiongozwa na Mwenyekiti wake Nahodha Mussa Mandia wameishauri Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) kuzingatia ratiba ya ujenzi wa MV Mwanza inayotarajiwa kukamilika mwezi Novemba,2022 baada ya kuona ujenzi wa meli hiyo unaendelea vizuri.

"Rai yetu kimsingi ni kuzingatia ratiba, muhimu kwao (MSCL) kuzingatia ratiba pia kuwa na mawasiliano ya mara kwa mara na mamlaka inayosimamia uundaji, ujenzi na uendeshaji wa vyombo vya majini TASAC", Nahodha Mandia alisema.

Nahodha Mandia ameyasema hayo baada ya Bodi hiyo kufanya ziara maalum ya ukaguzi wa ujenzi wa meli ya MV Mwanza, ili kujionea maendeleo ya mradi huo, kabla ya meli hiyo kukamilika na hatimaye kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

"Tumekuja hapa maalumu kwa ajili ya kuona mradi huu unaoendelea hapa Mwanza Kusini, mradi wa ujenzi wa meli ya abiria na mizigo maarufu kwa jina la MV MWANZA HAPA KAZI TU. Wenyeji wetu ambao ni MSCL wametutembeza wakishirikiana na wakandarasi ambao wapo kwenye shughuli hii ya ujenzi tumeweza kuona ni nini ambacho kinaendelea, kiasi gani meli imejengwa na kiasi gani kimebaki, mwishoni mwa mwaka kesho 2022 takribani mwezi wa 11 ni vema kutegemea meli hii ikiwa ipo tayari kuelea majini na kuweza kwenda katika safari ya kwanza ya majaribio", Nahodha Mandia alieleza.

Aidha, kwa upande wake meneja mradi wa MV Mwanza Ndg. Vitus Mapuda wakati akielezea changmoto za mradi huo alielezea kuwa miongoni mwa sababu zinazoathiri maendeleo ya ujenzi wa meli hiyo ni Ugonjwa wa Virusi vya Kovid (UVIKO-19)

"UVIKO-19 iliathiri mradi, meli nyingi zilikuwa hazifanyi kazi, na mizigo ya ujenzi wa meli hii inatoka pacific, inatoka Korea, kutoka Korea muunganiko wa safari hii ni lazima ipite ama Shanghai au Singapore ndio iweze kufika pwani ya Afrika Mashariki, kwahiyo kukawa na ugumu wa kupata kontena za kubebea mizigo", Mapunda alifafanua.

"Lakini ukija kwa upande wa watendaji, wahandisi wanatoka Korea, huko Korea kabla ya kuondoka walikuwa wanafungiwa kwa muda usiopungukiwa wiki mbili, wakifika hapa nchini wanafungiwa tena na hao wahandisi hawaji kwa wakati mmoja kwa sababu meli inajengwa na taaluma tofauti nyingi, kila watu wana taaluma zao na wana wakati wao waweze kufanya kazi, na inatakiwa muhandisi wa taaluma fulani atimize jukumu lake ndipo mwingine aweze kuja, hii ni njia nyingine iliyoathiri ujenzi wetu wa meli", Mapunda alisisitiza.

Meli ya MV Mwanza itakapokamilika itakuwa ya kisasa yenye uwezo wa kuchukua abiria 1200, mizigo tani 400 na magari 24 na itakuwa na daraja la kwanza, la pili, la tatu na VIP, ukumbi wa mikutano.

Meli Ya Mt. Sangara Kurudi Ziwa Tanganyika

Na Edmund Rutajama

Meli ya MT Sangara iliyotengenezwa mwaka 1980 na Kampuni ya Fulton Marine kutoka nchini Ubelgiji, imeanza ukarabati mkubwa utakaosababisha meli hiyo kutoka katika mfumo wa analogia na kuingia katika mfumo wa kidigiti ambao utaiwezesha meli kuwa na uwezo wa kisasa katika uendeshaji.

Ukarabati huo unaofanywa na mkandarasi, Kampuni ya KTMI ya nchini Korea Kusini utahusisha kubadili vifaa kadhaa ikiwemo mashine za pampu za mizigo (cargo pumps), injini, genereta na vifaa vya kuiongoza meli (Navigation equipments) ambapo ukarabati huo unahusisha shughuli zinazofanyika ndani na nje ya nchi.

Meneja wa mradi wa MT. Sangara Ndg. Kayuki Njenga wakati akizungumza na Meli TV alisema kuwa kuna matengenezo ya awali yaliyokwishafanyika katika kuboresha meli hiyo.

"Mpaka sasa hivi kuna matengenezo ambayo awali yameanza kufanyika ili kuboresha meli kutoka kwa mfumo wa zamani ambao ulikuwa unatumia shoteli mpaka kwa mfumo ambao ni 'direct proportion' na meli hii kufikia hapa tumeshafanya kitu kinaitwa 'Metal Still-Cutting' (ukataji wa vyuma), kazi ambayo inaendelea Korea Kusini na kuanzia mwezi wa 12 tutaanza 'site working' au 'site planning' ambayo itafanyika hapa hapa Kigoma kwenye meli yetu ya MT Sangara", Njenga alisema.

Kwa upande wake Nahodha Benjamin Titus alisema kuwa awali meli ya MT Sangara ilikuwa ikitembea kwa kiwango cha kasi ya nm 3, hivyo meli hiyo inatarajiwa kubadilishwa uwezo wake ili iweze kutembea kwa kiwango cha kasi ya nm 8 mpaka nm 10 pia, pia inatarajiwa kubadilishwa na kuboreshwa mfumo wa injini na upumuaji wake, ukarabati huo unatarajiwa kuleta manufaa makubwa na kuongeza ushindani kwa soko la ndani na nje ya nchi.

Hata hivyo, Nahodha Titus pia alitumia fursa hiyo kuzungumzia faida zitakazopatikana kutokana na ukarabati huo mkubwa na umuhimu wake katika soko la mafuta kupitia meli ya MT Sangara.

"Hizi injini mpya tunaweka sasa hivi itawezesha meli kufika kwa haraka kwenye vituo ambavyo tunapeleka mzigo , pia pampu tunaweka mbili mpya ambazo zitakuwa ni za umeme kwa sababu zamani tulikuwa tunatumia 'pump mechanical' sasa hivi tunaweka pampu za umeme ambazo zitawezesha uwezo wa kupakua mafuta utakuwa ni mkubwa sana, kwahiyo sababu zamani tulikuwa tunasafiri safari moja mpaka siku 8-10 kutoka Kigoma kwenda vituo vya Bunjumbura-Burundi, Uvira na Karemi(DRC-Congo) sasa hivi hali itabadilika," Alisema Nahodha Titus

Pia alifafanua kuwa soko la mafuta mkoani Kigoma ni kubwa na hivyo ukarabati wa meli hiyo utasaidia katika kutatua changamoto ya uwepo wa meli chache na hivyo kuiongezea mapato Kampuni na Serikali kwa jumla.

"Soko la mafuta Kigoma ni kubwa sana mpaka sasa hivi kuna meli ambazo zinakuja kupakia mafuta hapa, unakuta foleni imekuwa kubwa sana na meli ambazo zinafanya kazi ni mbili tu na mahitaji ya soko ni makubwa sana na haya mafuta ya kusafirisha kwenda nje ni mafuta ya dizeli na petroli" alisema.



Meli ya Mt. Sangara ikiwa imetia nanga bandari ya Kigoma katika Ziwa Tanganyika



Baharia Vicent Malegesi (wa kwanza kushoto) wa meli ya New Victoria Hapa Kazi Tu akitoa maelekezo ya namna ya kuendesha meli kwa wanafunzi wa kidato cha sita mkondo wa sayansi kutoka Sekondari ya Taqwa waliofika kujifunza mfumo wa uendeshaji wa meli

(Picha na Abdulrahman Salim 6.12.2021)

HABARI PICHA



Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Uhusiano kwa Umma Ndg. Anslem Namala akimsikiliza kwa makini mmoja wa wateja walioshindwa kuendana na ratiba ya meli nje ya uzio wa eneo la bandari ya Mwanza Kaskazini muda mfupi baada ya meli ya New Butiama kung'oa nanga kuelekea Nansio, Ukerewe. (Picha na Abdulrahman Salim 28.11.2021)

Baadhi ya Washindani wa mbio za mitumbwi walioshiriki katika mashindano ya mitumbwi yalioendeshwa na Kampuni ya The Scope na Kampuni ya Huduma za Meli kuwa miongoni mwa wadhamini wa mashindano hayo. (Picha na Abdulrahman Salim 12.12.2021)





Meli ya New Butiama Hapa Kazi Tu ikiwa imepandishwa kwenye Chelezo kwaajili ya ukaguzi, zoezi ambalo hufanyika kila baada ya mwaka mmoja tangu meli hiyo kutoa huduma.
(Picha na Abdulrahman Salim 29.10.2021)



Mmoja wa watumishi wa Kitengo cha Masoko na Uhusiano kwa Umma Bi. Fatina Msangi (kulia) akimkabidhi zawadi ya Krismas mmoja wa wateja waliokuwa wakisafiri na meli ya New Butiama wakati wa msimu wa sikukuu hiyo.

(Picha na Abdulrah-man Salim 26.12.2021)




Mmoja wa watumishi wa Kitengo cha Masoko na Uhusiano kwa Umma Bi. Sophia Chemponda (kulia) akimkabidhi zawadi ya Krismas kwa mmoja wa Watoto waliokuwa wakisafiri na meli ya New Butiama wakati wa msimu wa sikukuu hiyo.
(Picha na Abdulrahman Salim 26.12.2021)



Afisa wa Meli ya New Butiama Ndg.Kizito Mugyabuso akimlisha kipande cha keki mmoja wa wateja waliozawadiwa tiketi ya bure ya daraja la kwanza kwa safari ya kuwenda Nansio, Ukerewe. Tukio lili lofanyika kusheherekea wiki ya huduma kwa wateja inayofanyika wiki ya mwanzo ya mwezi Oktoba kila mwaka.
(Picha na Abdulrahman Salim 8.10.2021)

Uongozi wa MSCL wakagua maendeleo mradi wa Mt Sangara



Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya MSCL wakiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi hiyo Prof. Zacharia Mganilwa pamoja na watumishi wa MSCL tawi la mkoa wa Kigoma wakikagua mradi wa ukarabati wa meli ya MT. Sangara

Na Edmond Rutajama

Uongozi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) ukiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni hiyo Prof. Zacharia Mganilwa umefanya ziara ya kukagua maendeleo ya ukarabati wa meli ya mafuta ya MT Sangara katika bandari ya Kigoma katika Ziwa Tanganyika.

Akiongea baada ya kumaliza ukaguzi huo Prof. Mganilwa alisema kuwa Serikali ilitoa fedha na tayari mradi huo umekwishaanza kutekelezwa baada ya meli hiyo kusimama kutoa huduma tangu mwaka 2020 kutokana na uchakavu.

"Hali ya uchakavu ilisababisha mwendo kasi wa meli hiyo kushuka kutoka nm10 hadi kufikia nm 3 ambayo ni kasi ndogo zaidi, kushuka huko kulisababisha wateja wengi kutofurahia MT Sangara hivyo Serikali iliamua kutoa fedha ili kuikarabati meli hiyo," Alisema.

Prof. Mganilwa alieleza kuwa ukarabati huo unatarajiwa kuchukua takribani mwaka mmoja kukamilika ili kuweza kuhudumia wateja kwa ufanisi wa hali ya juu na kuongeza kuwa meli hiyo inatarajiwa kuwa miongoni mwa meli bora zaidi katika ukanda wa Ziwa Tanganyika.

Wakati huo huo Meneja Masoko na Uhusiano kwa Umma wa MSCL Bw. Anselm Namala ameizungumzia ziara hiyo kuwa ni yenye manufaa hasa kwa upande wa kitengo chake cha masoko kwani alibaini fursa kadhaa za kibiashara katika ukanda huo pamoja na kubaini maeneo ambayo kitengo hicho cha masoko kinatakiwa kujiimarisha na kuweka mikakati thabiti.

"Imekuwa ni ziara nzuri kwetu sisi watu wa masoko, kwa maana tumeona fursa zipo tumeona maeneo ambayo tumekuwa hatufanyi vizuri zile juhudi za kujitangaza kwetu katika eneo hili ni ndogo sana, kwahiyo itakuwa pia nafasi nzuri ya sisi kujitangaza, kuelezea shughuli tunazozifanya na sio kwa Kigoma na hata kwa matawi mengine", Alieleza.

Hata hivyo, alifafanua kuwa ziara hiyo imekuwa fursa kwa kitengo cha masoko kuweza kujipanga na kujitangaza zaidi ili wananachi waijue MSCL, wazitambue shughuli za Kampuni pamoja na kufahamu ujio wa meli ya MT Sangara, MV Liemba na MV muongozo na kufahamu shughuli zingine zinazofanyika ndani ya meli tofauti na usafiri na usafirishaji.


Kwa upande wake, Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa MSCL Ndg. Philemon Bagambilana alieleza kuwa Kampuni inatarajia kuwa mradi huo wa MT Sangara utakapokamilika utaleta mapinduzi makubwa katika utendaji wa Kampuni.

"Kukamilika kwa ukarabati wa MT Sangara tunatarajia utaleta mapinduzi makubwa katika usafirishaji, tunajua kabisa nchi za jirani Congo-DRC na Burundi kuna mahitaji makubwa sana ya kusafirisha shehena za mafuta na kwetu hii meli ya MT Sangara ni tegemeo kubwa kwa sababu gharama zake za usafiri ziko chini lakini pia huku ndio kujenga mahusiano mazuri na jirani zetu", Bangambilana alisema.

Aidha, Ndg. Bagambilana alipongeza juhudi za serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC) nchini kwa utekelezaji wa mpango wa ujenzi wa reli kutoka Mpanda kuelekea Karema pamoja na Mamlaka ya Bandari (TPA) kwa kutekeleza mradi wa ujenzi wa Bandari ya Karema katika Ziwa Tanganyika.

Mradi huo wa ukarabati wa meli ya MT Sangara wenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 8, unategemewa kumalizika baada yam waka mmoja huku mkataba wa mradi huo ukiwa umesainiwa mapema mwezi Aprili mkoani Mwanza , ukishuhudiwa na Bodi ya Wakurugenzi wa MSCL pamoja na wakandarasi KTMI kutoka Korea Kusini.

MV UMOJA YAKABIDHIWA KWA MKANDARASI TAYARI KUANZA UKARABATI



Kaimu Mhandisi Mkuu wa MSCL Mha. Abel Gwanafyo (wa pili toka kulia) akimkabidhi hati ya makabidhiano ya eneo la mradi wa ukarabati wa meli ya MV Umoja, Ndg. Jon Un Ye (wa pili toka kushoto) mbele ya Kaimu Mtendaji Mkuu wa MSCL Ndg. Philemon Bagambilana (wa tatu toka kulia)

Na Abdulrahman Salim

Menejimenti ya Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) imekabidhi rasmi eneo la mradi wa ukarabati wa meli ya MV Umoja kwa mkandarasi SM Solution kutoka nchi ya Korea Kusini ili kuanza ukarabati wa meli hiyo inayobeba mabehewa 19 kwa wakati mmoja.

Akizungumza wakati wa kukabidhi eneo hilo Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa MSCL alisema kuwa mkandarasi huyo ameshalipwa malipo ya awali na tayari ameshafanya maandalizi na hivyo kuwa na uwezo wa kuanza mradi huo

"Sasa tunamkabidhi rasmi eneo hili na meli husika ili kusudi aanze utekelezaji, kulikuwa na majadiliano ya mwisho ya kuhusu mambo ya kitaalamu ya masuala ya injini na utekelezaji wa mradi kwa jumla na nyaraka nyingine za kitaalamu ambazo tulikuwa tunakabidhiana, kwahiyo hiyo ndio inaashiria kwamba sasa mradi umeanza rasmi," Alimalizia.

Kwa upande wao kiongozi wa kampuni ya SM Solution Ndg. Jon Un Ye pamoja na mwakilishi mkaazi wa Kampuni hiyo Ndg. Reyton Kwembe wamesema kuwa siku hiyo ya makabidhiano ya eneo la kazi walikuwa wakiisubiri kwa hamu kwani tayari walikuwa wamefanya maandalizi yote muhimu kwa upande wao.

Aidha, aliongeza kuwa wameshafanya maandalizi ya kutosha kutoka nchini Korea Kusini yanapotoka malighafi kwaajili ya ukarabati wa meli hiyo pamoja na maandalizi ya eneo la kazi nchini Tanzania.

Akizungumzia changamoto ya uagizwaji wa vifaa hivyo Ndg. Kwembe alisema, "Ni kweli vifaa vyote vinaagizwa kutoka nje, kwasababu hapa hakuna kampuni inayotengeneza vifaa hivyo, kwa mfano kuna injini, mfumo wa uendeshaji, vifaa vya kuongozea meli, vyote vinaagizwa kutoka nchini Korea Kusini, lakini sisi tumejipanga hata kabla ya leo kukabidhiwa eneo, tayari tumeshaanza maadalizi ya kuagiza vifaa hivyo, kwahiyo baada ya kukabidhiwa na kupata uthibitisho, tutafanya uharaka wa kuagiza ili visichelewe kufika."

Mkataba wa ukarabati wa meli ya MV umoja ulisainiwa tarehe 15.6.2021 mbele ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan katika hafla fupi iliyofanyika bandari ya Mwanza Kaskazini. Mkataba ambao unathamani ya zaidi ya shilingi bilioni 20 na unategemewa kumalizika baada ya miezi 15.

Tutembelee kwenye mitandao yetu ya kijamii

Kampuni ya Huduma za Meli

mscltz MSCLtz Meli TV

SALAMU ZA MWAKA MPYA 2022

Heri ya Mwaka Mpya 2022

Napenda kuwatakia wafanyakazi wote wa Kampuni ya Huduma za Meli kila la heri katika mwaka huu wa 2022 ambao tunauanza sasa. Kama mnavyofahamu, mwaka 2021 umekuwa wa mafanikio mengi kwa taasisi yetu licha ya changamoto nyingi zilizojitokeza katika mwaka huo hususani janga la Ugonjwa wa Virusi vya Kovid – 19 (UVIKO -19) ambalo limeendelea kuitesa dunia nzima.

Kutokana na ushirikiano na mshikamano mkubwa tulioonyesha kwa pamoja katika mwaka uliopita, tulifanikiwa kuinua utendaji wa Kampuni kwa ujumla ikiwa ni pamoja na kufanya mambo yafuatayo: -

- Kuendelea na utoaji wa huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo kati ya Mwanza na Kemondo, Bukoba na Nansio - Ukerewe.
- Kukamilisha matengenezo ya meli ya MV Clarias kwa kutumia mapato ya ndani.
- Kuendelea na mradi wa ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza.
- Kukamilisha zoezi la uchambuzi wa madaraja ya watumishi (slotting).
- Kuidhinishwa kwa muundo mpya wa Kampuni.

Ni matumaini yangu kuwa tutaendeleza ari na mshikamano mkubwa katika kutekeleza majukumu ya Kampuni katika mwaka huu mpya wa 2022 ili kuendelea kukuza taswira ya taasisi yetu.

Aidha, Kampuni yetu imepanga kufanya mambo mengi katika mwaka huu ili kuunga mkono jitihada za serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan za kuwaletea maendeleo wananchi kupitia mapinduzi katika sekta ya uchukuzi. pamoja na mambo mengine Kampuni imepanga kufanya yafuatayo: -

- Kuanzisha safari mpya kati ya Mwanza na kisiwa cha Godziba kupitia kisiwa cha Gana kwa kutumia meli ya MV Clarias.
- Kuongeza idadi ya wasafiri na mizigo inayosafirishwa na meli za Kampuni ili kuongeza uzalishaji wa mapato.
- Kukamilisha miradi ya ujenzi wa meli ya MV Mwanza hapa kazi tu pamoja na ukarabati wa meli za MV Umoja na MT Sangara.
- Kuanza utekelezaji wa muundo mpya wa Kampuni.
- Kuboresha mifumo ya kielektroniki katika uendeshaji wa shughuli za Kampuni kama inavyoelekezwa na Serikali.

Ili kufanikisha mipango tajwa hapo juu na mingine mingi hatuna budi kuendeleza mshikamano, kujituma, upendo na ari ya utendaji kazi miongoni mwetu kwa manufaa ya taasisi na taifa kwa ujumla. Shime tuungane katika kuijenga taasisi yetu.

Nawatakia mwaka mpya wenye mafanikio tele kwa taasisi yetu pamoja na familia zetu.



Philemon N. Bagambilana
Afisa Mtendaji Mkuu (MSCL)

SHUKRANI ZA KIPEKEE KWA KUFANIKISHA JARIDA HILI

BODI YA WAHARIRI
MWENYEKITI – PHILEMON BAGAMBILANA

WAJUMBE
ANSELM NAMALA
BARAKA BIGAMBO
MHANDISI ABEL GWANAFYO
NAHODHA BEMBELE NG'WITA

MHARIRI MKUU

ABDULRAHMAN SALIM

JARIDA HILI IMEANDALIWA NA KUTOLEWA NA KAMPUNI YA HUDUMA ZA MELI

UJENZI WA MELI YA MV MWANZA WAFIKIA ASILIMIA 54

Na Mwandishi Wetu

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amesema ameridhishwa na hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa meli mpya ya MV. Mwanza inayotekelezwa katika Bandari ya Mwanza Kusini ambapo hadi sasa utekelezaji wake umefikia asilimia 54.

Prof. Mbarawa amezungumza hayo jijini Mwanza, katika ziara yake ya kikazi ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayoendelea na kuwataka wasimamizi wa mradi huo kuusimamia mradi huo ili ipatikane thamani ya fedha iliyotumika.

Prof. Mbarawa ameeleza kuwa ujenzi wa meli hiyo haujasimama kama taarifa zinazotolewa na watu wengine na kusisitiza kuwa msimamizi na mkandarasi wapo eneo la kazi usiku na mchana kuhakikisha meli hiyo inajengwa kwa viwango.

> **“Nimeridhishwa na kasi ya ujenzi wa meli hii na Serikali inaendelea kutoa fedha za mradi kwa wakati, hivyo mradi haujasimama kama watu wengine wanavyozusha”**
>
> **Prof . Mbarawa**

“Nimeridhishwa na kasi ya ujenzi wa meli hii na Serikali inaendelea kutoa fedha za mradi kwa wakati, hivyo mradi haujasimama kama watu wengine wanavyozusha”, amesema Prof. Mbarawa.

Ameeleza meli hiyo inayojengwa kwa gharama zaidi ya shilingi Bilioni 89 itakuwa na madaraja matatu, maeneo ya watu mashughuli (VIP), vyumba vya mikutano, uwezo wa kubeba abiria 1,200, tani 400 na magari madogo 20.

Aidha, ameeleza changamoto iliyokabili mradi huo kuchelewa ni kutokana na kuanza ujenzi wa meli bila ya kuwa na chelezo ambapo hadi sasa ujenzi wa chelezo umekamilika na kazi zinaendelea.

“Hii meli imechelewa kwa sababu moja tu huwezi kujenga meli na chelezo pamoja kwanza unaanza chelezo halafu unakuja kujenga meli”, amefafanua Prof. Mbarawa.

Akitoa taarifa ya mradi huo, Kaimu Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL), Ndg. Philemon Bagambilana, amesema kuwa ujenzi wa msingi wa meli hiyo kwa asilimia kubwa umekamilika na inatarajiwa kushushwa majini ifikapo mwezi Aprili au Juni huku ikiendelea kujengwa kwenye maji.



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa (wa pili toka kushoto) akiwa pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana Mhe. Amina Makilagi (kushoto) pamoja na Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu MSCL Ndg. Philemon Bagambilana (kulia) na Meneja Mradi wa MV Mwanza Ndg. Vitus Mapunda wakiendelea na ukaguzi wa ujenzi wa meli ya MV Mwanza katika bandari ya Mwanza Kusini.

Naye, Meneja wa Mradi Luteni Kanali Mhandisi Vitus Mapunda, amemuhakikishia Waziri kuwa ujenzi wa meli hiyo unasimamiwa kwa karibu kwa viwango vinavyohitajika katika meli za aina hiyo.



KAMPUNI YA HUDUMA ZA MELI (MSCL)

BANDARI YA MWANZA KASKAZINI, JENGO LA TPA, SAKAFU YA PILI
S. L. P. 2385, MWANZA, Hotline: +255 739 606 600
Barua Pepe: info@mscl.co.tz Tovuti: www.mscl.co.tz

Kampuni ya Huduma za Meli | MSCLtz | mscltz | Meli TV

JARIDA HILI IMEANDALIWA NA KUTOLEWA NA KAMPUNI YA HUDUMA ZA MELI NCHINI